HALIUZWI

# Jarida la NEMC

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 013 | OKTOBA - DISEMBA, 2023

# TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA UMOJA WA MATAIFA WA MABADILIKO YA TABIANCHI (COP28) 2023



Ndani:

- KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE MAJI NA MAZINGIRA YAIPONGEZA NEMC KWA USIMAMIZI WA SHERIA YA MAZINGIRA
- ELIMU YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA YATOLEWA KWA WADAU - GEITA
- MAZINGIRA NI FURSA YA KUJIKWAMUA KIUCHUMI

@nemctanzania NemcTVTanzania

#MazingiraYetuUhaiWetu

www.nemc.or.tz

# YALIYOMO


03 TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA UMOJA WA MATAIFA WA MABADILIKO YA TABIANCHI (COP28) 2023

04 CHUPA ZA RANGI NI CHANZO KIKUBWA CHA UCHAFUZI WA MAZINGIRA

05 KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE MAJI NA MAZINGIRA YAIPONGEZA NEMC KWA USIMAMIZI WA SHERIA YA MAZINGIRA

06 NEMC YASHIRIKI MAONESHO TAMASHA LA CHATO UTALII

07 WAZIRI JAFO AIPONGEZA NEMC KWA USIMAMIZI WA SHERIA YA MAZINGIRA MRADI WA JNHPP

08 TAKA NI FURSA KIUCHUMI, WEKEZA KATIKA TAKA SAFISHA MAZINGRA

09 ELIMU YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA YATOLEWA KWA WADAU - GEITA

10 HIVI NDIVYO TOPE SUMU LINAVYODHIBITIWA MIGODINI

11 NEMC YAICHARAZA MUCE BAO MBILI KWA MOJA MASHINDANO YA SHIMMUTA

12 TULINDE VYANZO VYA MAJI, TUTUNZE MAZINGIRA KWA MAENDELEO YA NCHI

13 NEMC YATOA ELIMU YA MAZINGIRA TAMASHA LA UTALII VISIWA VYA MAFIA

14 MAZINGIRA NI FURSA YA KUJIKWAMUA KIUCHUMI

15 NEMC YATOA SIKU SABA KWA KIWANDA CHA CHANZI LIMITED KUDHIBITI UCHAFUZI WA MAZINGIRA

15 NEMC YABAINI UKIUKWAJI WA SHERIA YA MAZINGIRA BANDARI YA DAR ES SALAAM

16 NEMC YASIMAMIA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KUHIMILI MABADILIKO YA TABIANCHI TANZANIA BARA NA VISIWANI

18 WAZIRI JAFO ATOA RAI KWA WANANCHI KUSHIRIKI KATIKA KUHIFADHI TABAKA LA OZONI

19 ATHARI ZA VITUO VYA MAFUTA KWENYE MAKAZI YA WATU

20 KAULI YA MAZINGIRA


## UTANGULIZI

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria hiyo Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira; na
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.


**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
**Dkt. Menan Jangu**

**Mhariri Mkuu:**
**Irene John**

**Wachangiaji:**
Dalia Charles
Rose Mtui
Martha Kawishe
Tajiri Kihemba
Nana Elias
Boniphace Kyaruzi

**Msanifu Michoro:**
Blasius Haule

# TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA UMOJA WA MATAIFA WA MABADILIKO YA TABIANCHI (COP28) 2023



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Seleman Jafo akiwa katika moja ya mikutano iliyofanyika katika Mkutano wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) 2023 Dubai Falme za Kiarabu.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Seleman Jafo amekutana na waandishi wa habari kwa ajili ya kutoa mrejesho wa mkutano wa Nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai Falme za Kiarabu kuanzia tarehe 30 Novemba hadi 12 December 2023.

Akizungumza na waandishi hao wa habari Desemba 18, 2023 katika ukumbi wa mikutano wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Jafo alisema lengo la COP28 lilikua ni kupitia taarifa mbalimbali, kufanya tathmini, majadiliano na maamuzi kuhusu hatua zilizochukuliwa na Nchi wanachama katika kufikia malengo ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Itifaki ya Kyoto pamoja na Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi. Ujumbe Mkuu wa COP28 ilikuwa "Unite, Act, Deliver". Kaulimbiu hii ililenga kuzitaka nchi wanachama wa Mkataba kuungana na kutekeleza kwa pamoja Sera, Mipango na Mikakati ya mabadiliko ya tabianchi.

Waziri Jafo amesema mkutano huo ulihudhuriwa na washiriki takribani 110,000 kutoka Nchi mbalimbali duniani. Kwa upande wa Tanzania washiriki walikua ni Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikua kiongozi mkuu wa ujumbe akiongozana na viongozi wengine; waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wataalamu na wawakilishi kutoka Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia. Kulikua na jumla ya washiriki 50 kutoka Serikalini zikiwemo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, washiriki 8 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wabunge 3 na washiriki 300 kutoka sekta binafsi, Asasi za Kiraia ikiwemo vijana na Watoto walishiriki.

Aidha Mhe. Jafo amethibitisha kuwa kupitia Mkutano wa COP28 Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania itanufaika zaidi na fedha za miradi, teknolojia, utaalam na Programu mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo Programu ya Afrika ya Nishati Safi ya Kupikia; programu ya Afya na mabadiliko ya tabianchi; na utekelezaji wa mikakati ya kuimarisha uhimili katika katika sekta ya Maji, Misitu na Bahari.

Dkt. Jafo pia ameufahamisha Umma kupitia mkutano huo na Waandishi wa habari kuwa Mkutano wa 29 (COP29) umepangwa kufanyika Azerbaijan 11 – 22 Novemba, 2024 na Mkutano wa 30 (COP30) utafanyika Nchini Brazil tarehe 10 – 21 Novemba, 2025.



# CHUPA ZA RANGI NI CHANZO KIKUBWA CHA UCHAFUZI WA MAZINGIRA



*Pichani ni chupa za rangi zilizotupwa baada ya kutumika na kusababisha uchafuzi wa mazingira*

Chupa za plastiki za rangi hasa nyeusi zinazotumika kuhifadhia vinywaji vya kuongeza nguvu (energy drinks) zimekuwa zikizagaa maeneo ya mijini ikiwemo Dar es Salaam jambo ambalo linazidisha uchafuzi wa mazingira.

Utupaji hovyo wa chupa hizo unasababisha kuziba kwa mitaro, muonekano mbaya wa mitaa, uchafuzi wa vyanzo vya mji ikiwemo mito na bahari. Pia huchangia kuharibu rasimali bahari na vifo vya viumbe vyake.

Chupa hizo zinakuwa nyingi mtaani kutokana na vinywaji vyake kutumika kwa wingi na hali hiyo imesababisha taka za plastiki kutapakaa kwenye mazingira, na kuwa sehemu kubwa ya mabaki nchini, jambo ambalo linazidisha uwezekano wa kutokea mafuriko kipindi cha mvua kutokana na mifereji inayosafirisha maji ya mvua kuziba.

Kutokana na athari za chupa za plastiki kwenye mazingira, ni dhahiri kuwa juhudi zinahitajika ili kupunguza chupa za plastiki za rangi mitaani kama ilivyofanyika kwenye chupa angavu ambazo hutumika kuhifadhia maji ya kunywa.

Waokotaji chupa za plastiki wameomba kampuni zinazotengeneza chupa hizo kuzibadilisha rangi ili waweze kuziokota na kujipatia kipato, vilevile kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Wadau wa mazingira wanashauri kuwa ni vyema kwa makampuni husika kuanzisha mfumo wa kuzikusanya chupa za rangi baada ya kuzitumia ili zitumike tena.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) likiwa kama chombo kinachosimamia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kupitia Mkurugenzi Mkuu wa Baraza Dkt. Samuel Gwamaka limeagiza wazalishaji wote wa vinywaji vinavyowekwa kwenye chupa za rangi kuhakikisha wanazirejeleza chupa hizo ili ziweze kutumika tena ili kuondoa changamoto ya kuzagaa kwa chupa hizo mitaani na kusababisha madhara kwenye mazingira na viumbe hai.

Endapo wazalishaji wa chupa za plastiki za rangi watatekeleza maagizo ya Serikali na wenye viwanda vya urejelezaji chupa za plastiki kutumia teknolojia ya kisasa itasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na chupa hizo.

***"Kuna wimbi kubwa la uchafuzi wa mazingira kutokana na chupa za rangi za vinywaji, sisi kama Baraza tunawataka wamiliki wa viwanda vya chupa zenye rangi kuwa na miundombinu au utaratibu wa kurejeleza taka hizo ili kulinda na kutunza mazingira. Hivyo tunatoa mwezi mmoja kuanzia leo Novemba 7, 2023 kukamilisha baada ya hapo tukigundua hujafuata utaratibu hatua za kisheria zitachukuliwa."***

Alisema Dkt. Samuel Gwamaka.

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE MAJI NA MAZINGIRA YAIPONGEZA NEMC KWA USIMAMIZI WA SHERIA YA MAZINGIRA



*Kamati ya Kudumu ya Bunge Maji na Mazingira wakiwa katika ziara ya kikazi ya ukaguzi wa utekelezaji wa maagizo ya Serikali kuhusu mazingira katika kiwanda cha kutengeneza chuma na nondo cha lodhia kilichopo Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani.*

Kamati ya Kudumu ya Bunge Maji na Mazingira chini ya Makamu Mwenyekiti wake Mhe. Anna lupembe (Mb) imelipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa usimamizi na utekelezaji mzuri wa Sheria ya Mazingira.

Pongezi hizo zimetolewa na kamati ya Kudumu ya Bunge maji na Mazingira wakiwa katika ziara ya kikazi ya ukaguzi wa utekelezaji wa maagizo ya Serikali kuhusu mazingira, yaliyotolewa kwa kiwanda cha kutengeneza chuma na nondo cha lodhia kilichopo Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani.

''Kiwanda hiki kilikuwa na uchafuzi mkubwa wa hewa unaotokana na mitambo kutoa moshi mwingi, hali iliyokuwa ikiathiri wakazi wa eneo husika pamoja na mazingira, lakini kwa sasa tunaona kwa macho hali ni nzuri udhibiti wa hewa chafu umefanyika, udhibiti wa kelele zitokanazo na mitambo umefanyika, udhibiti wa utupaji hovyo wa taka hatarishi umefanyika, hii maana yake ni kwamba NEMC wamefanya kazi yao kwa ufasaha zaidi na elimu ya mazingira imeenea, hongereni sana NEMC" Alisema Mhe. Anna Lupembe (Mb).

Aliongeza kuwa ni vema pia wawekezaji wakazingatia ushauri unaotolewa na wataalamu wa Mazingira hasa suala la ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya uendelezaji wowote ili kuepuka changamoto za kimazingira hasa ikizingatiwa utunzaji wa mazingira kwa wawekezaji kote nchini ni jambo la kuzingatiwa kwani azma ya Mhe. Rais Mama Samia ni kuendeleza uwekezaji na kutunza Mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Naye waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo ameishukuru kamati ya kudumu ya Bunge Maji na Mazingira kwa ziara hiyo ya ukaguzi wa utekelezaji wa maagizo ya Serikali kwa kiwanda cha Chuma na Nondo Wilayani Mkuranga na kuwataka wawekezaji wengine kuiga mfano mzuri wa utunzaji wa mazingira kutoka kwa Mwekezaji Lodhia.

Kadhalika Mkurugenzi wa Kiwanda cha Nondo, Chuma na Plastiki Ndg. Sailesh Pandit alipokuwa akipokea maelekezo na ushauri kutoka kwa kamati ya bunge, ameahidi kuyatekeleza kwa wakati na kulinda mazingira kwa mstakabli wa maendeleo endelevu ya Taifa na pia kutoa ajira kwa vijana wa kitanzania hasa wanawake ili kukuza uchumi wa viwanda.

Ziara hiyo imehudhuriwa na kamati ya maji ya bunge, kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya ya Mkuranga, Menejimenti ya NEMC pamoja na wadau wa mazingira.



# NEMC YASHIRIKI MAONESHO TAMASHA LA CHATO UTALII

Tamasha la Chato Utalii, ni mwendelezo wa Maonyesho ya Biashara na Utalii yaliyoanzishwa mwaka 2021 Wilaya ya Chato, mwaka huu limechukua nafasi kubwa katika kutangaza vivutio vya utalii, fursa za uwekezaji, bidhaa, na kuibua vipaji. Lengo kuu lilikuwa kukuza ukuaji wa uchumi, sio tu kwa watu binafsi ndani ya wilaya ya Chato bali kwa taifa zima.

Hii inakuwa ni mara ya pili kufanyika kwa Maonesho ya Utalii Wilaya ya Chato, kufuatia tukio la uzinduzi mwaka 2021, ambalo lilishuhudia washiriki zaidi ya 400, wakiwemo wa ndani na nje ya nchi. Maonyesho hayo yalivutia wageni 30,000, na kuleta athari kubwa katika Hifadhi ya Taifa ya Burigi na Kisiwa cha Rubondo, huku zaidi ya raia 360 wa Tanzania wakichagua kuchunguza maajabu hayo ya asili.

Tamasha la Chato Utalii 2023 lilisisitiza dhamira ya Halmashauri ya Wilaya ya Chato katika kukuza utalii. Tamasha hilo lilifanyika kwa kasi kubwa, likihusisha shughuli zilizopangwa kama vile kutembelea maeneo ya burudani ndani ya wilaya ya Chato, mafunzo ya ujasiriamali, michezo na burudani mbalimbali zikiwemo Chato Utalii Marathon, mbio za baiskeli, ngumi, mpira wa miguu na boti za mbio za maji (mashindano ya mitumbwi). Ngoma za kitamaduni ziliongeza msisimko wa kitamaduni kwenye sherehe hizo.

Maonesho ya Chato Utalii yalizinduliwa tarehe 26 Novemba, 2023 na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe Abdallah Hamis Ulega. Mhe. Ulega alitumia fursa hiyo kukagua miradi mbalimbali inayohusu uvuvi, ufugaji, soko la kimataifa na hoteli ya nyota tatu inayoendelea kujengwa hivi sasa. Katika hotuba yake ya ufunguzi, aliwataka wananchi kutumia ipasavyo rasilimali zilizopo na kueleza nia ya dhati ya kuwekeza katika sekta ya utalii.

Baraza la taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kama kiungo kikuu kati ya wawekezaji na wananchi kwa ujumla katika masuala yanayohusu utunzaji wa mazingira lilishiriki katika maonesho hayo. Lengo kuu la ushiriki wa Baraza lilikuwa ni kutoa huduma kwa umma juu ya masuala yote yanayohusu Utunzaji na Uhifadhi na mazingira. Malengo mengine ni; Kutoa elimu juu ya taratibu na umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) kabla ya kuanzishwa kwa miradi yoyote ya maendeleo, kupokea maoni, ushauri na malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali na kuyashughulikia, kuhakikisha wananchi wanafahamu usimamizi wa taka hatarishi, kuongeza uelewa juu ya Katazo la matumizi ya plastiki, na ukuzaji wa uelewa juu ya teknolojia rafiki (cynadation) inayotumika kuchenjua madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo (ASGM).

Kupitia maonesho hayo, Baraza lilipata fursa ya kutoa mawasilisho katika mikutano mbalimbali ya wadau iliyoandaliwa ambapo , Afisa Sheria wa Baraza Mr. Vincent Haule aliweza kutoa ufafanuzi wa Majukumu ya Baraza pamoja na Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya usimamizi wa mazingira. Aidha Afisa Sheria huyo alifanikiwa kutoa ufafanuzi zaidi katika mambo muhimu yafuatayo; umuhimu wa kufanya Tathmini ya Atahari kwa Mazingira na Jamil (TAM), Katazo la mifuko ya plastiki, udhibiti wa taka ngumu (utenganishaji wa taka kwenye chanzo ili ziweze kuwa rahisi kurejelezwa au kutumika kwa matumizi mbadala ), udhibiti wa taka hatarishi na matumizi ya teknolojia mbadala wa zebaki katika uchimbaji wa madini ya dhahabu.



Katika monesho hayo.

Vilevile Baraza kupitia wataalamu wake kutoka Kanda ya Ziwa, lilianda banda la maonesho ambapo wageni mbalimbali walitembela katika banda hilo ili kupata elimu ya utunzaji wa mazingira. Kupitia fursa hiyo Baraza lilifanikiwa kutoa elimu ya Uhifadhi na Utunzaji wa mazingira kwa ujumla kwa wadau mbalimbali waliowatembelea kwa siku saba (7) katika banda la NEMC kuanzia tarehe 26 Novemba hadi 3 Desemba 2023, pia wadau walipata fursa ya kuyatambua majukumu ya Baraza, kujua umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kama sharti kabla ya kuanza mradi wowote na athari zinazoweza kujitokea ikiwa maradi umeanzishwa pasipo kukufanya Tathmini ya Athari kwa Mazngira na Jamii.

Wataalamu wa NEMC wakiwa katika banda la NEMC kwenye maonesha ya Chato Utalii yaliyofanyika Wilaya ya Chato Mkoa wa Geita

NEMC ilipata bahati ya kutembelewa na Waziri wa Madini, Mhe. Anthony Mavunde, ambaye alieleza kusikitishwa na kutokuwepo kwa ofisi ya NEMC Mkoani Geita. Katika ziara yake Mhe. Mavunde alipongeza utendaji wa jumla wa NEMC katika utekelezaji wa majukumu yake. Alitambua jukumu muhimu lililofanywa na NEMC katika kulinda mazingira na kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake. Utambuzi huo wa Waziri ulisisitiza umuhimu wa michango ya NEMC katika kuzingatia viwango vya utunzaji wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira.

Baadhi ya viongozi walipo tembelea banda la NEMC na kupata elimu ya utunzaji wa mazingira kwenye maonesha ya Chato Utalii yaliyofanyika Wilaya ya Chato Mkoa wa Geita

Vilevile wageni wengine waliotembelea bandani walipa nafasi ya kuweza kutoa maoni au ushauri juu yakuboresha utendaji wa Taasisi na maoni hayo yalipokelewa na kufikishwa katika ngazi husika kwa utekelezaji. Pia wadau waliweza kutoa malalamiko yao kuhusu mapungufu ya utendaji wa Baraza na baadhi ya malaamiko yalipata ufumbuzi wa papo kwa papo na mengine yakapelekwa katika ngazi husika kwa hatua zaidi.

# WAZIRI JAFO AIPONGEZA NEMC KWA USIMAMIZI WA SHERIA YA MAZINGIRA MRADI WA JNHPP



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe Dkt. Seleman Jafo (wa katikati) akiongea na waandishi wa habari alipotembelea Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (JNHPP).*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Seleman Jafo amelipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa usimamizi mzuri wa Sheria ya Mazingira katika mradi wa kufua umeme wa bwawa la Mwalimu Nyerere (JNHPP).

Pongezi hizo zimekuja mara baada ya Waziri huyo kuzuru eneo la mradi akiambatana na Bodi ya wakurugenzi kwa lengo la kujiridhisha na hatua za ujenzi zilipofikia sambamba na suala la Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira katika eneo hilo.

"Mradi huu ni mkubwa wenye shughuli kubwa na nyingi zinazozalisha taka za kila aina na idadi ya watu takribani 12,000, hutegemei kukuta mazingira nadhifu kama haya, hizi zote ni juhudi za Baraza la Mazingira ambalo lilipiga kambi kabisa hapa kuhakikisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inasimamiwa hasa ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Hongereni sana " Alisema Mhe. Jafo.

Aidha Mhe. Jafo amesisitiza utunzaji wa vyanzo vya maji ya mto Kilombero, Luwege na Ruaha na kuzitaja faida za mradi huu wa kufua umeme wa bwawa la Mwalimu Nyerere kuwa ni upatikanaji wa umeme wa uhakika, udhibiti wa mafuriko, uanzishwaji wa kilimo cha maji, kupunguza nishati ya kuni na mkaa na kuongeza ujuzi kwa wataalamu wa Nchi yetu.

Nyingine ni ongezeko la mapato kwa Serikali, upatikanaji wa maji, kuanzisha utalii wa maji kwa njia ya boti pamoja na kutunza ikolojia ya hifadhi ya mbuga ya selou.





# TAKA NI FURSA KIUCHUMI, WEKEZA KATIKA TAKA SAFISHA MAZINGRA



*Pichani ni mapambo yaliyotengenezwa kutokana na chupa zilizotumika*



*Pichani ni vifaa chakavu vya kielekroniki vilivyokusanywa kwa ajili ya urejelezaji.*

Taka au kama wengine wanavyoita Takataka ambazo huonekana au kuchukuliwa kama uchafu kutokana na hali yake mbaya isiyovutia machoni au wakati mwingine zinaambatana na harufu mbaya hasa kwa zile taka zitokanazo na mabaki ya chakula, watu wengi huzidharau na kuona si kitu.

Lakini ukweli ni kwamba licha ya kukosa mvuto machoni, uchafu wake na wakati mwingine harufu mbaya itokanayo na uchafu au kuoza kwa taka hizo, ukweli ni kwamba taka ni fursa kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja, kampuni na hata Taifa kwa ujumla.

Mnyororo wa thamani wa taka unaweza kunufaisha watu wengi kuanzia mkusanyaji wa taka, ,msafirishaji wa taka, mtenganishaji taka kutokana na mahitaji lakini pia mzalishaji wa bidhaa au huduma itokanayo na taka.

Kitu wasichokijua watu ni kuwa kutokana na takataka zinazozalishwa maeneo mbalimbali kuna watu hujiingizia kipato cha uhakika, ni biashara inayohitaji mtaji na haina hasara. Kitu muhimu ambacho watu hawakifahamu ni namna ya kutenganisha taka hizo kutoka kwenye chanzo ili kuweza kukidhi matumizi. Kuchanganya taka za aina tofauti tofauti ndiko kunakowakosesha wengi fedha kwani zinapoteza sifa za kutumika tena.

Ili kuziongezea thamani taka ni vizuri kuzitenganisha kutokana na aina ya taka mfano zinazooza na zisizooza ili kurahisisha uhifadhi, usafishaji na matumizi ya taka hizo kama malighafi, soko la taka lipo lakini utenganishaji wa taka kutoka kwenye chanzo ndio utakaokupatia kipato. Wakusanya taka wanapozichukua kutoka majumbani au sehemu nyingine tofauti tofauti huzitofautisha kwa kuziweka kila aina ya taka katika sehemu yake kabla ya kuzipeleka kuziuza kwa wateja wao ambao huzitumia kwa matumizi mbadala au kuzirejereza na kutengeneza bidhaa nyingine mbalimbali.

Faida kubwa ya taka ni kurejelezwa na kutengeneza bidhaa au vitu vipya mfano karatasi nyeupe hutumika kutengenezea karatasi zinazotumika chooni na kujifuta mikono au kushikia vitu (tissue-paper), maboksi hutumika kutengeneza bidhaa kama trei za mayai wakati vyuma mbalimbali hutumika kutengeneza nondo na bidhaa nyingine za vyuma na mabaki ya chakula, matunda na mbogamboga hutumika kutengeneza mbolea na vyakula vya mifugo kama funza.Vilevile taka hutumika kutengezea mapambo na mikekaya aina mbalimbali mfano taka za plastiki, matairi ya gari n.k

Fursa nyingine ni fursa ya taka za kielektroniki ambazo hutokana na bidhaa za kielekroniki zilizoharibika au kuisha muda wa matumizi na kuonekana hazifai kwa matumizi kama vile televisheni, redio, nyaya, kompyuta na vifaa vingine vingi vya kielekroniki. Taka hizi pia hurejelezwa na kutengeneza tena bidha nyingine za kielektroniki kwa ajili ya kutumika upya.

Hakuna taka ambayo haiwezi kununuliwa ni vile tu watu wengi hawajapata kujua vizuri biashara ya taka na kama wataijua vizuri na mifumo mizuri ya ukusanyaji na urejelezaji wa taka ngumu ukizingatiwa kwa usahihi katika jamii itatunza mazingira, pia itakuwa chanzo cha ajira kwa vijana nchini na Duniani kwa ujumla. Hivyo ni vema kuzingatia mifumo mizuri ya urejelezaji wa taka ngumu ili vijana waweze kupata fursa ya kujiajiri kupitia taka.

# ELIMU YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA YATOLEWA KWA WADAU - GEITA




*Viongozi wa NEMC wakitoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu namna na umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Jamii, madhara ya afya kutokana na matumizi ya Zebaki.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na STAMICO, limetoa elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa wachimbaji wadogo katika Maonesho ya sita (6) ya Kimataifa ya Madini yaliyofanyika katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere Mkoani Geita.

Akitoa elimu hiyo kwa wachimbaji wadogo, mratibu wa mradi wa zebaki Bi Befrina Igulu amesema ni vizuri kabla uchimbaji wowote, wazingatie ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira ili kuweza kunusuru mazingira ya baadae na kulinda afya na ikolojia ya Mazingira pia.


Mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uelewa wachimbaji wadogo kuhusu namna na umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Jamii, madhara ya afya kutokana na matumizi ya Zebaki, matumizi sahihi ya Zebaki na njia Mbadala za uchenjuaji bora kwa kutumia Zebaki.

Sambamba na hilo Baraza liliendesha majadiliano na wadau mbalimbali kwa lengo la kuwapa mwanya wa kuweza kutoa maoni na mapendekezo lakini pia kubadlishana uzoefu wa utekelezaji wa majukumu kutoka katika Taasisi nyingine ili kuweza kuboresha utendaji wa Baraza.



*Wachimbaji wadogo wakipata elimu kuhusu namna na umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Jamii, madhara ya kiafya na kimazingira kutokana na matumizi ya Zebaki.*

# HIVI NDIVYO TOPE SUMU LINAVYODHIBITIWA MIGODINI



*Pichani ni Bwawa la kuhifadhia tope sumu katika mgodi wa Barrick wa Bulyankulu uliopo Kahama Mkoani Shinyanga*

Tope sumu ni tope linalozalishwa baada kuchimba na kuchenjua madini kama vile Dhahabu, Shaba, Almasi, Bati, Lisasi n.k upatikanaji wake hutumia kemikali ambazo ni hatari na sio rafiki kwa Mazingira ikijumuisha ardhi, uoto, wanyama na maji (maji ya uso na chini ya Dunia -. Hali hiyo hupeleka tope hilo kuwa na mchanganyiko wa kemikali mbalimbali ambazo hutofautiana kutokana na jiolojia ya mahala madini yalipopatikana na njia ya uchenjuaji iliyotumika

Ili kuweza kudhibiti tope hilo lisisambae na kuleta madhara kwa viumbe hai na mazingira, wamiliki wa migodi ni vema wakazingatia taratibu za ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhia tope sumu (Tailing Storage Facilities). Bwawa la kuhifadhia tope sumu ni muundo mbinu unaojengwa kitaalamu kwa ajili ya kuhifadhia tope sumu zinazozalishwa baada ya kuchenjua madini. Mabwawa ya tope sumu pamoja na mabwawa ya maji kwa ujumla yanahitaji umakini katika utengenezaji na usimamizi kwa usalama wake.

Pia ni muhimu kwa wamiliki kuwa na teknolojia ya kufuatilia usalama wa mabwawa haya. Usalama usipozingatiwa kuna uwezekano wa mabwawa kufurika, kuvuja au kupasuka na kuleta madhara makubwa katika mazingira na kuhatarisha afya na maisha ya jamii.

Vilevile Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) ni lazima ifanyike kabla ya ujenzi wa bwawa la tope sumu na mabwawa ya maji ili kuweza kupata cheti kilichoambatana na masharti pamoja na mpango wa usimamizi wa mabwawa hayo kutoka NEMC kwa lengo la kuepuka ujenzi usiozingatia vigezo na kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza wakati uendishaji.

Kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira ni jukumu la kila mwananchi taifa ikiwa na kauli mbiu ya kudumu isemayo; ***"Tunza mazingira yakutunze"*** ni muhimu sana na takwa la kisheria kwa miradi yote ya madini ambayo iko kwenye kundi la matumizi ya **kemikali** kuhakikisha inajenga **Bwawa la kuhifadhia tope sumu** linalotokana na uchenjuaji wa madini husika.

**Ujenzi wa Bwawa la Tope Sumu** unatakiwa kuzingatia **utaalamu, uadilifu na sheria**, ili kuhakikisha ujenzi wa bwawa lenye ubora unaokidhi viwango takikana. Kuna aina tatu za mabwawa kulingana na usanifu

a) Mkondo juu

b) Mkondo chini Mkondo kati

**Mambo muhimu ya kufanya kabla ya kujenga Bwawa**

Mchakato wa kujenga bwawa ni muhimu na unalazimu kufanya mambo kadhaa kabla ya kuamua ni aina gani ya bwawa lisanifiwe (to be designed) ambayo ni;

i. Kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira

ii. Kufanya utafiti wa kijiologia katika ploti pangwa (Geotechnical study on planned plot);

Utaafiti huu utajibu mambo mbalimbali muhimu kwa usalama wa bwawa, ikiwa ni pamoja na;

a) Muonekano wa juu wa uso wa dunia (topography);

b) Mipasuko ya miamba chini ya aridhi (natural faults);

c) Mitetemo ya asili (natural seismic vibration);

d) Tabia za udongo (Soil Properties i.e. porosity, modulus); n.k.

iii. Kufanya utafiti wa maji ya uso na chini ya uso wa dunia.

Utafiti huu utajibu mambo makuu matatu ambayo ni:-

a) Maji ya uso wa Dunia;

b) Mikondo ya maji chini ya uso kina kifupi); na

c) Maji ya kina kirefu chini ya uso

Taarifa hizi zitaamua usanifu na ujenzi wa bwawa. Izingatiwe kuwa ujenzi wa bwawa la **mkondo juu (upstream)**. Pia hairuhusiwi katika maeneo yenye mitetemko mikubwa

**Ujenzi wa Bwawa**

Ujenzi wa bwawa, ili kuhakikisha kimiminika chenye sumu hakipenyi kuingia ardhini na hakibaki kwenye bwawa ambacho huchangia kubomoa kuta za bwawa pamoja na kutakiwa kujenga ukuta imara ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Kufanya usanifu na kuchora michoro ya bwawa na kuidhinisha kwa mamlaka zinazohusika;

ii. Kuondoa undogo wote wa juu kwa kuzingatia usanifu;

iii. Kukandamiza kitako na kuta za bwawa);

iv. Weka matandiko ya kuzuia kimiminika kupenya kwenda ardhini;

v. Jenga mfumo wa kukusanya kimiminika katikati ya bwawa;

vi. Jenga mfumo wa kukusanya kimiminika pembezoni ya bwawa kwa kiminika ambacho hakikuelekea kwenye penstock system;

vii. Jenga mfumo wa kumwaga tope sumu kuzunguka bwawa lote (tailings discharge spigot system); na

viii. Weka mifumo ya kusimamia usawa wa

Inaendelea Uk. 11

# NEMC YAICHARAZA MUCE BAO MBILI KWA MOJA MASHINDANO YA SHIMMUTA

Timu ya mpira wa miguu ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imeiadhibu timu ya Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) bao mbili kwa moja katika mashindano ya michezo ya SHIMMUTA yanayoendelea katika viwanja vya Jamuhuri Mkoani Dodoma.

Katika mtanange huo uliodumu kwa takribani dakika 90,kwa mapumziko ya dk 45 za kwanza NEMC ilijipatia bao la kwanza kutoka kwa mwanamazingira machachari Bw.Fortunatusi Patriki kwa shuti kali iliyopenyeza lango la MUCE katika dakika ya tatu ya mchezo baada ya kumzunguka beki wa kati wa timu ya MUCE wakati bao la pili la ushindi lilipatikana dakika ya 10 kutoka kwa mhandisi Msafiri Laurent na kuiweka NEMC katika nafasi nzuri ya ushindi wa bao moja dhidi ya MUCE.

Nao MUCE katika kujitafuta dakika 22 walifanikiwa kupata bao la kufuta machozi kupitia mchezaji wao Mwinyi Ramadhani na kufanya mechi hiyo kumalizika kwa NEMC kupata ushindi wa magoli mawili kwa moja.

Katika mchezo huo pia MUCE walipata penati ambayo haikuzaa matunda baada ya mchezaji wao kushindwa kutamba mbele ya golikipa Tajiri Kihemba.


NEMC wamemaliza michuano hiyo wakiwa nafasi ya tatu hatua ya makundi upande wa mpira wa miguu kwenye kundi lenye timu tano ambazo ni TPA, Ngorongoro, TTCL, MUCE na NEMC yenyewe.



*Kikosi cha Timu ya Mpira wa miguu ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wakiwa katika picha ya pamoja kabla ya mchezo wao dhidi ya Kikosi cha MUSE.*

*Inaendelea Uk. 10*

## HIVI NDIVYO TOPE SUMU ...




*Picha 1: Usanifu wa aina ya mabwawa tope sumu*

tope sumu kwenye bwawa.

### Usimamizi wa Bwawa la tope sumu

Usimamizi wa bwawa ni muhimu na unahitaji utaalamu na uadilifu mkubwa kwa maana inawezekana hatua zote za utafiti wa eneo zimefanyika vizuri zikasaidia usanifu wa bwawa bora na ujenzi makini na imara ukafanyika lakini usimamizi ukiwa mbaya ni sawa na kazi bure. Hivyo ni muhimu usimamizi kuwa mzuri ili kuwezesha bwawa kuwa salama na kuishi muda uliopangwa ili kulinda mazingira na kuokoa garama kubwa endapo bwawa likiharibika (Tailings storage facility failure).

Ili kuhakikisha bwawa liko salama wakati wote na linatoa matokeo tegemewa yafuatayo ni muhimu sana kusimamiwa kwa udilifu mukubwa;

Kuhakikisha usawa wa tope sumu kwenye bwawa.

i. Kuhakikisha tope sumu linawekwa kwa mteremko kiasi kueleka katikati ya bwawa ili kuruhusu kimiminika kutiririka kwa mvuto
ii. Kuhakikisha kimiminika kinachovunwa kinarudishwa kwenye mfumo wa uchenjuaji;
iii. Kuhakikisha wakati wote bwawa ni kavu kutokea ukutani na kavu kiasi kuelekea katikati ambako kimiminika kinachujwa;
iv. Kuhakikisha mfumo wa kuchuja kimiminika unafanya kazi vizuri wakati wote;
v. kuhakikisha mfumo wa kukusanya kimiminika pembezoni ya bwawa kwa kiminika ambacho hakikuelekea kwenye penstock system unafanya kazi vizuri;
vi. Kuhakikisha kina cha maji sumu hakivuki ukuta wa asili (starter wall);
vii. Kuhakikisha hakuna kimiminika chochote kinapenya kwenda ardhini

### Baadhi ya mifumo ya usimamizi wa bwawa la tope sumu (TSF)

Ipo mifumo ya usimamizi wa bwawa la tope sumu imegawanyika katika nyanya kuu mbili ambazo ni Manual na Automatic systems.

Mifumo isiyo ya moja kwa moja (manual) ni :-

Nguzo ya mti/zege yenye vipimo vya usawa (Levels) zinazosimikwa kuzunguka bwawa kwa umbali sawa na linapotolewa tope sumu kwenda kwenye bwawa kusaidia kuangalia mtawanyiko sawia wa tope sumu; na

Mfumo wa kisasa wa piezometer ya bomba la kusimama, kusaidia kupima kina cha maji.

Mifumo ya moja kwa moja (automatic) ni:-

Piezocone mfumo wa kisasa kwa kuangalia usawa, kina cha maji na mkandamizo hasi (pore pressure / negative pressure); na

Piezometer inayotetemeka (vibrating piezometer) mfumo wa kisasa kwa kuangalia kina cha maji.

# TULINDE VYANZO VYA MAJI, TUTUNZE MAZINGIRA KWA MAENDELEO YA NCHI



Ni dhahiri kwamba sote tunatambua umuhimu wa maji katika kuendesha maisha ya mwanadamu, na ni ukweli usiopingika kuwa viumbe vyote vinategemea maji ili viweze kuishi. Viumbe hai hutegemeana na hapo ndipo umuhimu wa maji unapoonekana kuwa wa kiwango kikubwa. Maisha ya wanyama yanategemea sana maji, mimea na hewa ili kuishi, vivyo hivyo maisha ya mimea yanategemea maji na hewa katika uhai wake.

Tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa mijini na vijijini ni kero kubwa hasa wakati wa kiangazi kutokana na uharibifu mkubwa unaofanywa katika vyanzo vya maji kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu ambao kimsingi haukubaliki hata kidogo kwani hurudisha nyuma juhudi za Serikali katika kulinda vyanzo vya maji na kuhakikisha wananchi wanapata maji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Uharibifu wa vyanzo vya maji na mfumo wa maji ni miongoni mwa changamoto za mazingira zinazoendelea kulikabili Taifa letu. Pamoja na jitihada za Serikali za kukabiliana na changamoto hizo, hatua zaidi zinahitajika kuhakikisha hali hiyo inadhibitiwa na kukomeshwa.

Jukumu la kutunza vyanzo vya maji ni la kila mtu kutokana na umuhimu wake katika jamii kwani vyanzo hivyo vya maji ndivyo vinavyotupatia maji kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama uendeshaji wa viwanda, shughuli za kilimo cha umwagiliaji, ufugaji na shughuli nyingine za nyumbani. Hivyo kutokana na umuhimu huo, kila mwananchi ana wajibu wa kutunza vyanzo vya maji ili kuweza kupata maji kwa ajili ya mahitaji ya kila siku.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) linaendelea kutoa rai kwa watanzania kila mmoja kwa nafasi yake kuendelea kutunza vyanzo vya maji na kuwa mabarozi wazuri wa utunzaji wa Mazingira kwani tusipotunza mazingira tunahatarisha vyanzo vyetu vya maji na kupelekea athari mbalimbali kama vile njaa, mlipuko wa magonjwa na kushuka kwa kiwango cha uzalishaji nchini hali inayopelekea kushuka kwa uchumi uchumi wa Nchi na mtu mmojammoja.

# NEMC YATOA ELIMU YA MAZINGIRA TAMASHA LA UTALII VISIWA VYA MAFIA




*Mkuu wa Mkoa Mhe. Abubakari Kunenge akifungua tamasha la utalii lililofanyika katika visiwa vya Mafia Mkoani Pwani*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC limeshiriki tamasha la utalii lililofanyika katika visiwa vya Mafia Mkoani Pwani kwa kutoa elimu ya Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira kwa wananchi wa Mafia.

Tamasha hilo lililofunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhe. Abubakari Kunenge lenye kauli mbiu isemayo "Gundua visivyojulikana" limelenga kuzitangaza fursa zilizoko Pwani zitakazowavutia si tu watalii bali wawekezaji ili kukuza uchumi wa Nchi.

"Hili tamasha kufanyika hapa si kwa bahati mbaya, litafungua fursa za uchumi wa buluu kwani visiwa vya Mafia vina vivutio vingi vya uwekezaji." Amesema Mhe.Kunenge

Naye Afisa Mazingira Mwandamizi - NEMC Bw. Gifti Ngowo alipozungumza amesema ili kufanyike uwekezaji mkubwa na endelevu katika sekta ya Utalii wa bahari na uvuvi, ni lazima Mazingira yatunzwe na kuhifadhiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake.



*Afisa Mazingira Mwandamizi - NEMC Bw. Gifti Ngowo akitoa elimu ya Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira kwa mwananchi aliyetembelea katika banda la NEMC tamasha la utalii lililofanyika katika visiwa vya Mafia Mkoani Pwani.*

# MAZINGIRA NI FURSA YA KUJIKWAMUA KIUCHUMI



Mazingira ni vitu vyote vinavyozunguka wanadamu kwa mfano miti, mito, maziwa, bahari, nyumba na kadhalika. Vitu vyote hivi vinapoizunguka jamii vikiwa katika hali ya usafi na kutunzwa hupendezesha muonekano wa mahali kwa mvuto wenye afya unaotamanisha kuangaliwa mara kwa mara.

Nchi ya Tanzania kwa nyakati tofauti, kupitia matamko ya viongozi, Sera, Sheria, mitazamo imekuwa ikisisitiza na kufafanua umuhimu wa Kutunza na Kuhifadhi Mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa kwani ni fursa inayoweza kumkwamuwa mwananchi kutoka hali duni na kufikia hatua ya maendeleo.

Ni siku za hivi karibuni tu mtazamo wa muda mrefu uliokuwepo kwamba suala la mazingira ni jambo la kuchelewesha maendeleo umeanza kubadilika. Hii inatokana na ukweli kuwa uharibifu wa mazingira umekuwa dhahiri na kuathiri maisha ya wananchi hasa wale maskini zaidi. Mabadiliko haya yamesaidia kuongeza hali ya usikivu na tahadhari miongoni mwa wanasiasa juu ya umuhimu wa kuwa mazingira bora kwa maisha ya watu, afya, kukua kwa uchumi na usalama.

Lakini pia kumekuwa na mabadilko ya uelewa na utambuzi hasi kuhusu suala la utunzaji wa mazingira inayotokana na fikra potofu ya kibinadamu kwa misingi ya kukabiliana na fursa za kiuchumi hali inayopelekea changamoto katika kuyatunza na kuyahifadhi mazingira kwani umaskini na uharibifu wa mazingira ni watoto mapacha na mama yao ni ujinga.

Ikitazamwa hata katika Miongozo na Sera ya Mazingira ya mwaka 1997 imeainisha matatizo makuu sita ya mazingira yanayoikabili nchi yetu. Matatizo haya ni: Uharibifu wa ardhi na kutopatikana kwa maji safi kwa wakazi wa mjini na vijijini, Uchafuzi wa mazingira na upotevu wa makazi ya viumbe – pori na bioanuai, Uharibifu wa makazi ya viumbe wa majini, na Uharibifu wa misitu

Matatizo hayo yaliyoainishwa katika Sera ya Mazingira kwa tafsiri rahisi ni zile shughuli za kibinadamu zinazofanyika kinyume na Sheria ya Mzingira na kupelekea uharibifu wake. Shughuli hizo za kibinadamu ni kama vile kulima pembezoni mwa vyanzo vya maji, kukata miti hovyo ili kupata mbao na kuni, kutiririsha maji machafu kwenye mkondo wa maji safi, kutumia vifungashio visivyo na sifa kwa lengo la kufungia bidhaa, kutupa chupa za plastiki hovyo, kupiga kelele mitaani, kutiririsha mafuta machafu na hewa chafu kutoka viwandani hali inayoathiri hali ya hewa na kufungua gereji bubu kwenye maeneo ya makazi.

Shuhguli hizo za kibinadamu zinazofanyika hupelekea changamoto za kimazingira ikiwemo athari za mabadiliko ya Tabia Nchi, kupotea kwa uoto wa asili, mafuriko, ukame, changamoto za kiafya kutokana na kuharibiwa kwa tabaka la ozone pamoja na uharibifu wa miundombinu kama barabara kutokana na mafuriko .

Lakini jamii ya watanzania yapaswa kuondokana na mitazamo hasi inayoongozwa na hisia pamoja na tamaduni za makabila hasa zile zinazoshinikiza uharibifu wa mazingira kama kuchoma misitu, n.k na kuhakikisha wanatumia mazingira kama fursa ya kujikwamua katika chamgamoto za uchumi.

Fursa hizo ni pamoja na taka ngumu kama magurudumu ya magari kuwa na uwezo wa kubadilishwa na kutengeneza meza au viti vinavyoweza kutumika tena, makopo ya plastiki na vyuma chakavu kutengeneza mapambo mbalimbali yanayotumika katika maeneo mbalimbali, kupanda miti na kuuza, kupanda ukoka na kupendezesha lakini ukauza pamoja na kuokoa viumbe hai vya majini kama samaki kwa kutumia njia sahihi za kuvua ili kulinda ikolojia ya majini na kutunza mazingira. Lakini pia taka za plastiki zinaweza kurejelezwa hali hii husaidia kuondoa taka zinazozagaa mitaani na kutoa fursa ya kiuchumi kwa wananchi wanaookota aina hii ya taka mitaani na kwenda kuziuza kwa warejelezaji.vilevile taka ngumu huweza kutumika kuzaliza nishati mbadala kama mkaa na taka zile zinazooza huweza kutumika kama malighafi kwa ajili ya kuzalia mbolea kwa ajili ya kuapndia mazao mbalimbali.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dk. Selemani Jafo amekuwa akisisitiza sana masuala ya utunzaji wa Mazingira kuwa fursa za kiuchumi hasa kwa vijana kwani bado kuna changamoto zinazoikumba sekta ya mazingira kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo huathiri uhai wa viumbe hai na misitu na kuwataka vijana kutumia fursa hizo kujiongezea kipato.

Amekuwa akiyasisitiza haya kupitia mikutano na majukwaa mbalimbali ya kimazingira yanayojadili namna bora ya kutumia fursa mbalimbali zinazotokanazo na utunzaji wa mazingira.

Ni wito kwa vijana kuiokoa nchi isiingie kwenye jangwa kwa kufanya ubunifu wa vitu mbalimbali kama ambavyo Serikali imeweka kipaumbele kwa vijana katika kusaidia taifa kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

# NEMC YATOA SIKU SABA KWA KIWANDA CHA CHANZI LIMITED KUDHIBITI UCHAFUZI WA MAZINGIRA



Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limetoa siku saba kwa Kampuni ya Chanzi Limited inayojishughulisha na uzalishaji wa funza kwa ajili ya utengenezaji wa chakula cha mifugo, kuhakikisha wanazuia harufu kali inayotokana na shughuli zinazofanyika kiwandani hapo ili kuondoa kero kwa wananchi na kulinda Mazingira

Agizo hilo limetolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria - NEMC Dkt. Thobias Mwesiga Richard alipozuru eneo la tukio na kubaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira hali iliyosababisha uharibifu wa hali ya hewa na kuleta kero kwa wananchi.

"Tumefanya ukaguzi katika eneo hili na tumejiridhisha kwamba kweli changamoto hiyo ipo, na changamoto yenyewe ni harufu kali inayotoka hapa ambayo inawaathiri wakazi wa maeneo haya na sisi maelekezo yetu kama Baraza ni kwamba kwanza kiwanda hiki kihamishiwe eneo lingine mbali na makazi ya wananchi, eneo ambapo hakitaathiri hali ya hewa na kukera wananchi" Amesema Dkt. Thobias.

Aidha Dkt. Mwesiga amemtaka Mwekezaji kuhakikisha anadhibiti harufu hiyo mbaya kwa haraka wakati akiendelea kufuatilia kukamilika kwa mchakato utakaomuwezesha kuhamisha kiwanda chake eneo la makazi ili kuwaondolea kero wananchi na kulinda mazingira.


Naye Bi. Mayasa ambaye ni Meneja wa Kampuni ya Chanzi limited alipozungumza amekiri kuwepo kwa kero hiyo na kuahidi kutekeleza agizo hilo kwa wakati ili kunusuru afya za raia wa eneo hilo na kulinda Mazingira.

# NEMC YABAINI UKIUKWAJI WA SHERIA YA MAZINGIRA BANDARI YA DAR ES SALAAM

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC limebaini ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa taka hatarishi ya mwaka 2021 unaotokana na ukataji wa taka hatarishi eneo la dockyard KOJ bandari na kupelekea kutiririsha mafuta na taka nyingine baharini.

Akiongea katika eneo la dockyard KOJ bandari ambako mabomba ya mafuta ya makampuni mbalimbali yanapita Dkt. Thobias Mwesiga, Kaimu Mkurugenzi idara ya Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira NEMC amesema utiririshaji wa mafuta kuelekea baharini ni kinyume cha Sheria na kinahatarisha uhai wa viumbe wa baharini pamoja na uchafuzi wa Mazingira na kuyataka makampuni yaliyohusika kuchukuliwa hatua za kisheria pamoja na kurejesha mazingira katika hali yake.

"Sisi kama Baraza tumefanya ukaguzi wa kushtukiza katika eneo la Bandari ya Dar es Salaam eneo la dockyard KOJ ambalo ni eneo yanakopita mabomba ya mafuta ya makampuni mbalimbali, tumebaini ukataji wa taka hatarishi kinyume cha matakwa ya Sheria unaopelekea uvujaji mkubwa wa mafuta yanayotiririka kuelekea baharini na kuathiri viumbe hai wa baharini. Huu ni ukiukwaji mkubwa wa Sheria na Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa Taka hatarishi (Hazardous Waste regulation ya mwaka 2021) Maelekezo yetu Kama Baraza, Makampuni yaliyobainika kufanya makosa hayo kuitwa na kuchukuliwa hatua pamoja na kuhakikisha yanarejesha mazingira katika hali yake.



*Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira NEMC Dkt.Thobias Mwesiga akitoa maelekezo kwa bandari ya nama ya kurejesha mazingira katika hali ya awali eneo la dockyard KOJ kutokana na ukiukwaji wa utirirshaji wa mafuta na taka nyingine.*

# NEMC YASIMAMIA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KUHIMILI MABADILIKO YA TABIANCHI TANZANIA BARA NA VISIWANI



*Pichani ni sehemu ya tuta lililojengwa kwa ajili ya kupunguza adha ya maji kuingia kwenye mabonde yanayotumika kwa shughuli za kilimo katika eneo la Tovuni Shehia ya Kiungoni, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba*

Mabadiliko ya tabianchi ni miongoni mwa changamoto kubwa ambayo inachangia kudhoofisha maendeleo ya nchi kiuchumi, kijamii na kimazingira. Mabadiliko ya Tabianchi husababishwa haswa na shughuli za binadamu ikiwemo uvunaji wa misitu usiokuwa endelevu, ongezeko la viwanda Duniani ambavyo mfumo wa uzalishaji na matumizi yake kama vile mitambo hutoa hewa ukaa. Vilevile mabadiliko hayo husababishwa na kilimo, ufugaji, makazi, uchomaji moto wa misitu na mbuga n.k.

Tanzania ni miongoni mwa Nchi iliyoathirika na Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, kutokana na athari hizo zimepelekea kuanzishwa kwa miradi sehemu mbalimbali Tanzania Bara na Visiwani ili kuweza kuhimili athari hizo. Kwa upande wa Tanzania bara miradi hiyo inatekelezwa katika maeneo ya Mikoa ya Dodoma (Kongwa, Bahi), Singida (Manyoni), Tabora (Nzega, Igunga) na Mara (Bunda). Tanzania Visiwani miradi hiyo inatekelezwa katika maeneo ya Bubwini (Shehia ya Makoba,Mafufuni na Kidogo- Wilaya ya Kaskazini B, Mkoa wa Unguja) na kwa upande wa Pemba unatekelezwa katika eneo la Tovuni Shehia ya Kiungoni, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Miradi hiii inafadhiliwa na Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation fund), na inatekelezwa chini ya usimamizi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za mitaa katika maeneo husika ambapo mradi huo unatekelezwa. Aidha, utekelezaji wa miradi hii ni kutumia fursa ya NEMC ya kupata ithibati na mfuko wa Adaptation Fund, na hivyo jukumu lake ni kuisadia Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuandaa na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kuhilimili mabadiliko ya tabia nchi. Lengo la Miradi hii ni kujenga uwezo wa wakulima wadogo kuweza kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa njia za vitendo na ubunifu ambazo zitakuwa na matokeo yenye tija.

**Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabiachi kwa wakazi wa pwani nchini Zanzibar**

Malengo ya mradi;

1. Ujenzi wa Mabwawa yenye uwezo wa kusambaza maji kwa mwaka ikiwa na lengo la kuboresha upatikanaji wa maji kama uvunaji wa mabwawa ya mvua na kuanzishwa kwa mifumo ya umwagiliaji maji yenye ufanisi kwa kutumia mifumo ya dripu.
2. Kukuza mbinu za uhifadhi wa udongo na maji kwa ajili ya kuboresha udhibiti wa maji na uzalishaji mazao ili kuboresha usimamizi wa ardhi ili kuboresha mavuno ya mazao na kuboresha usimamizi wa vyanzo vya maji.
3. Kuanzisha shughuli mbadala za kijamii zinazohimili mabadiliko ya tabianchi ili kukuza vitalu vya miti kwa ajili ya kusambaza miche, kuboresha ufugaji wa kuku kupitia vikundi vya wafugaji, kujenga mabwawa ya ufugaji wa samaki, kuboresha ufugaji wa nyuki na kuongeza uzalishaji bora wa mazao ya kilimo cha mbogamboga.
4. Kujenga uwezo kwa mamlaka za serikali za mitaa na jamii ili kujenga uwezo wa serikali za mitaa juu ya masuala ya kilimo stahimilivu na kuimarisha uwezo wa jumuiya za wakulima na jamii katika kukuza utekelezaji wa kilimo stamilivu

**Hatua ilipofikia mpaka sasa;**

1. Tuta lenye urefu wa mita 400 la kuzuia uingiaji wa maji ya bahari limejengwa katika bonde la mpunga la Tovuni, Shehia ya Kiungoni, Wilaya ya Wete, Pemba.
2. Kuwajenga uwezo jumla ya wanajamii 69 (35 wanaume na 34 wanawake) wa Shehia ya Tovuni, Makoba, Mafufuni na Kiongwe Kidogo kwa kupatiwa mafunzo ya ufugaji wa nyuki endelevu. Aidha, wanajamii 50 (25 wanaume na 25 wanawake) wamepatiwa mafunzo ya upandaji na uhifadhi wa Mikoko na miti ya juu.
3. Ujenzi wa msingi ya maji mvua (Drainage Canal) katika eneo la Tovuni.
4. Kukamilika kwa hatua za awali za ujenzi wa bwawa na la kuhifadhia maji katika eneo la Machekechuni, Shehia ya Mafufuni. Hatua hizo ni pamoja na:
    - Kupatikana kwa eneo la ujenzi wa bwawa la maji lenye ukubwa wa 0.76 hekta pamoja na kufanya 'demarcation' zake.
    - Kutayarishwa kwa ramani (engineering drawing) za bwawa la maji, Gharama za ujenzi (BoQ), Nyaraka za Zabuni, Ripoti ya Tathmini ya Athari za Kimazingira na kupatikana Mkandarasi wa Ujenzi

Mradi wa kukabiliaa Mabadiliko ya Tabianchi Wilaya ya Kongwa

Malengo ya mradi

1. Kusaidia upatikanaji wa maji ya uhakika wa wakulima na wafugaji katika kata za ugogoni na mtanana;
2. kuwezesha shughuli za wananchi ziwe endelevu na ziweze kuhimili mabadiliko ya tabia ya nchi;
3. kutunza mazingira ili yaweze kuwalinda wananchi dhidi ya mabadiliko ya tabia ya nchi; kujenga uwezo wa tasisi na maofisa katika wilaya ya kongwa juu ya namna bora ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi ili kuepuka majanga yanayoweza kujitokeza
4. Kutunza mazingira ili yaweze kuwalinda wananchi dhidi ya mabadiliko ya tabia ya nchi;
5. Kujenga uwezo wa tasisi na maofisa katika wilaya ya Kongwa juu ya namna bora ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi ili kuepuka majanga yanayoweza kujitokeza.

Hatua ilipofikia mpaka sasa;

1. Kuchimba visima viwili vya maji
2. Kujenga matanki 2 ya kuhifadhi maji
3. Kujenga mtandao wa kusambaza maji wa kilometa 1 wenye vichoteo 4 (drawing points)
4. Kujenga vinywesheo 2 vya kunyweshea mifugo pamoja takribani 300 kwa mkupuo
5. Kujenga josho 1
6. Kufufua makingamaji yaliyokuwepo tangu enzi za ukoloni ili kuhifadhi maji na kukuza kilimo endelevu katika eneo la eka 100
7. Kupanda miti ya matunda na mbao, pamoja na mbegu bora ya nyasi za kulishia mifugo
8. Kujenga mfumo wa nishati ya jua kwa ajili ya kusukuma mashine ya kusambaza maji vijijini
9. Kutoa mbegu bora za ng'ombe kwa wananchi

Mradi wa uvunaji maji wa kimkakati kuwezesha uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa wakazi wa vijijini kwenye sehemu kame za katikati ya Tanzania, Mikoani dodoma, Singida na Tabora

Malengo ya mradi;

1. Kujenga na kukarabati mabwawa ya kuvuna maji ili kuwezesha shughuli za kilimo, mifugo, pamoja na kuchimba visima vya maji kwa matumizi ya binadamu;
2. Kuandaa na kutekeleza mpango shirikishi wa upandaji miti ya matunda, kuni, mbao na kuanzisha vitalu vya miti;
3. Kuwezesha shughuli mbalimbali za kujiongeza kipato na ktk njia inayozingatia uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kama vile upandaji miti, uanzishaji wa vitalu vya miti, ufugaji wa samaki, nk;
4. Kuandaa na kutekeleza mbinu za kukabiliana na wadudu waharibifu na magonjwa ya mifugo na mimea yanayojitokeza kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi ili kuboresha uzalishaji wa kilimo na mifugo

Hatua ilipofikia mpaka sasa;

1. Kufanya tathmini ya ardhi katika maeneo ya mabwawa na kusafisha mazingira ya bwawa,
2. Kuchimba na kukarabati Mabwawa 5 ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua
3. Kupanda miti kwenye madakio ya mabwawa ili kuyahifadhi mabwawa
4. Kuanzisha na kusimamia vitalu vya miti katika jamii
5. Kuchagua na kukusanya aina ya miti inayostahimili mazingira ya nyanda kame zilizopo kwenye mradi
6. Kuboresha wa mbinu za kuzalisha miti ya matunda na misitu inayostahimili maeneo ya ukame
7. Kupanda wa miti ya misitu na matunda katika mashamba na ardhi iliyoathirika na mabadiliko ya tabia nchi
8. Kutunzan na Usimamizi wa miti iliyo pandwa
9. Kuanzisha na kunza mazao ya bustani
10. Kuweka miundombinu ya umwagiliaji wa bustani
11. Kuanzisha vitalu vya mboga, na bustani za mboga pamoja na miundo mbinu ya kuvutia nyuki wa kuchavusha mazao bustani (pollinators)
12. Kutengeneza manywesheo ya mifugo na mabomba ya kupeleka maji
13. Kutoa mafunzo na semina za matumizi endelevu ya maji katika mabwawa kwa wakazi wa maeneo ya mradi
14. Kuunda vikundi na kutoa mafunzo ya uanzishaji na utunzanji wa vitalu vya miti
15. Kujengea jamii uwezo wa utunzaji na upandaji wa miti ya misitu na matunda kama chanzo cha kipato

Mradi wa kuhimili mabadiliko ya Tabianchi Wilayani Bunda, Mara

Malengo ya mradi;

1. Kukarabati miundombinu ya maji na kupanua wigo wa mtandao maji vijijini;
2. Kuchimba visima vya maji kwa maeneo yasiyo karibu na vyanzo;
3. Kuwezesha shughuli mbadala za kuinua vipato vya wananchi kama vile kutengeneza miundimbinu ya kilimo cha umwagiliaji, ufugaji wa samaki, kuku, nyuki nk;
4. kupanda miti ya matunda, mbao na kuni na kuhifadhi mifumoikolojia iliyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi;
5. Kutoa elimu ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa wananchi na viongozi wa halmashauri ya wilaya.

Hivyo basi kwa wanufaika wa mradi huu wanapaswa kuutumia mradi huu vizuri kwa kuhakikisha zile athari za Mabadiliko ya Tabianchi zinapungua, kuongeza uzalishaji wa mazao kupitia umwagiliaji unaotokana na ujenzi wa mabwawa na pia kuongeza uzalishaji wa miche ya mikoko na miti ya juu kupitia vitalu vitakavyozalisha miche. Kama mradi huu utatekelezwa ipasavyo basi utapelekea kuendelea kupata misaada katika mfuko wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi (Adaptation fund).





*Pichani ni kitalu cha miti na bwawa la maji kwa ajili ya kuwezesha kilimo cha umwagiliaji, hii ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kukabiliana na Athari ya Mabadiliko ya Tabianchi Wilaya Manyoni Singida.*

# WAZIRI JAFO ATOA RAI KWA WANANCHI KUSHIRIKI KATIKA KUHIFADHI TABAKA LA OZONI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Selemani Jafo (MB.) ametoa rai kwa wananchi kuacha matumizi ya vifaa vinavyoharibu tabaka la Ozoni kwani madhara yake ni makubwa.

Ameitoa kauli hiyo alipokuwa akiongea na waandishi wa habari katika ukumbi wa mikutano wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Jijini Dodoma ikiwa ni siku chache baadae ambapo Tanzania itaungana na Jumuia ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni Septemba 16, 2023.

Amesema Tabaka la Ozoni linatakiwa kulindwa kwani linapoharibiwa huruhusu mionzi ya jua kufika kwenye uso wa dunia na hivyo kusababisha ongezeko la magonjwa mbalimbali yakiwemo saratani ya ngozi, mtoto wa jicho, upungufu wa kinga dhidi ya maradhi, kujikunja kwa ngozi, kuathirika kwa ukuaji wa mimea na kuongezeka kwa joto duniani  kunakochangia katika mabadiliko ya tabianchi

“Katika utekelezaji wa mkataba wa Montreal tulitoa maelekezo na kutoa mafunzo kupitia mipaka yetu kupiga marufuku ya gesi, friji au viyoyozi vilivyotumika. Ukiangalia mwaka juzi kuna kazi mbalimbali zilikuwa zikifanyika kwa watengenezaji hasa wa friji na kwenda katika maduka ili kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa mafundi ili waweze kujua madhara yake,” amesema Dkt. Jafo.

Ameongeza kuwa mafunzo hayo yalilenga namna ya kudhibiti uingizaji wa kemikali nchini pamoja na namna bora ya kukarabati vifaa hivyo pasipo kuachia angani kemikali na hivyo kuharibu mazingira kwa Maafisa wa Idara za Serikali zilizopo katika Mpaka wa Namanga.

Kadhalika yalilenga kutoa elimu kwa wanafunzi wa fani ya viyoyozi katika Chuo cha Ufundi Arusha pamoja na mafundi wa viyoyozi na majokofu kwa mkoa wa Arusha.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Hifadhi ya Tabaka la Ozoni na Kupunguza Athari za Mabadiliko ya Tabianchi” yenye lengo la  kuchangia jitihada za kuhifadhi tabaka la ozoni na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Selemani Jafo (MB.) akiongea na vyombo vya Habari kuelekea Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni.*

# ATHARI ZA VITUO VYA MAFUTA KWENYE MAKAZI YA WATU



Makazi ya binadamu ni mazingira ambayo binadamu huishi, huingiliana na kuzaliana. Na makazi hayo huzungukwa na mazingira mazuri yenye nyumba za kuishi, miti mizuri, hewa safi na salama, miundombinu bora ya barabara na maeneo ya huduma muhimu za jamii kama hospitali, shule, nyumba za ibada na maeneo ya kibiashara yaliyotengwa kwa mujibu wa Sheria ya Mipango miji.

Makazi haya yanahitaji usalama wa kimazingira kwa usaidizi wa maisha ili mwanadamu aweze kuyafikia malengo yake ya kuishi kwa afya na ustawi. Usalama wa Mazingira unaotajwa ni ule wenye kuzuia au kurekebisha uharibifu wa mazingira, kuzuia au kukabiliana na migogoro inayosababishwa na mazingira na kulinda mazingira kutokana na thamani yake ya kimaadili.

Na ili makazi ya mwanadamu yaweze kufikia sifa tajwa ni lazima mamlaka husika zifanye kazi kwa pamoja ili kuona nama ya kusimamia Sheria husika katika kuhakikisha makazi ya mwanadamu yanakuwa salama siku zote anapoishi.

Lakini kwa tafsiri hiyo katika jamii ya Tanzania ni kama inapotea, wananchi kwenye makazi wamekuwa wakiishi mazingira hatarishi bila hatua zozote kuchuliwa hali inayowaathiri kiafya kutokana na chanzo kinachohatarisha mazingira hayo kutokuchukuliwa hatua au kuzuiwa kabisa.

Kumekuwa na ongezeko kubwa la ujenzi holela wa vituo vya mafuta katikati ya Miji na maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia Sheria ya Mazingira na Mipangomiji pamoja na mamlaka husika kama EWURA kwa ajili ya vibali au leseni za biashara hiyo hali inayohatarisha maisha ya wakaazi wa maeneo husika.

Ikumbukwe kwamba vituo hivi vinavyojengwa katikati ya makazi ya watu vinahudumia magari makubwa kwa madogo, vinahifadhi nishati ya mafuta na wakati mwingine vinageuzwa parking ya magari makubwa na madogo, vinapokea malori makubwa ya mafuta na wakati mwingine bila kuzingatia miundombinu ya barabara hali inayoweza kuzalisha foleni na ajali zisizokuwa za msingi.

Hali hii huleta athari ya uchafuzi wa hali ya hewa kwani mafuta ya petroli au dizel wakati wa kumiminwa kwenye visima au kujazwa kwenye magari yana harufu inayotapakaa na kuchafua hali ya hewa hali inayopeleka kuwashwa koo, kuumwa tumbo, kichefuchefu, kutapika, kizunguzungu na maumivu ya kichwa na kusababisha changamoto ya kiafya kama magonjwa ya mfumo wa hewa mfano TB, PUMU, pamoja na magonjwa ya mafua.

Baadhi ya madhara mengine ya mafuta kwa maisha ya mwanandamu pale yanapoguswa kwa ukaribu hupelekea kuwashwa, vipele, uwekundu na uvimbe na yanapoachwa wazi kwa muda mrefu pia hupelekea kuzimia au kufa. Kadhalika vituo hivi huweza pia kusababisha msongo wa mawazo na kupelekea hali kuwa mbaya kwa kushindwa kulala kutokana na kelele za magari zinazosababishwa na vituo hivyo wakati wa kujaza mafuta kwenye kisima na magari.

Ikumbukwe pia mafuta haya ni nishati inayochochea moto unaoweza kulipuka wakati wowote, kwa mstakabali huu ni hatari kwa vituo hivi kujengwa kwenye makazi ya watu kwani yaweza kuleta athari ya moto na kusababisha madhara makubwa ikiwemo kupoteza maisha ya watu, nyumba pamoja na rasilimali nyingine.

Kadhalika vituo hivi vya mafuta vinapojengwa eneo la makazi huharibu miundombinu ya barabara kwani haina uwezo wa kubeba tani kubwa za magari ya mafuta hali inayoweza kupelekea foleni na mwisho ajali.

Lakini pia vituo hivi vinapojengwa kwenye makazi ya watu ni chanzo kikuba cha kelele kutokana na magari kupita na kuwek mafuta,na kuifanya jamii inayoisi eneo husika kuwa na kutokusikilizana kwa kukosa utulivu.

Ni majira sahihi sasa kwa vyombo vyenye dhamana ya Sheria kama Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sheria ya Mipangomiji, chombo chenye dhamana ya Mazingira kwa kusimamia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake na wale wenye malaka za kutoa vibali vya mafuta kuingilia kati suala hili ili kujiridhisha kama ujenzi huu umezingatia vigezo vyote vya kisheria ikiwemo ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM), kwani hutoa muongozo wa namna sahihi ya kuenenda katika kukamilisha mradi wowote bila kuleta athari za Kimazingira, hasa ujenzi wa vituo hivi vya mafuta katikati ya makazi ya watu.

# Kauli ya Mazingira Yetu

### KAULI YA MAZINGIRA YETU
JUMATATU 27, NOVEMBA 2023




"Nyasi zinapopandwa shambani husaidia kutunza unyevunyevu katika ardhi (evaporation) ili maji yasipotee kwa njia ya kuvukizwa wakati jua linapowaka hasa kiangazi. Panda nyasi tunza unyevunyevu shambani.

### KAULI YA MAZINGIRA YETU
JUMATANO 29, NOVEMBA 2023



"Nyasi husaidia kuzuia mmomonyoko wa udongo kwani zinapopandwa shambani hupunguza kasi ya maji na kufanya ardhi ibaki na udongo wa kutosha. Hivyo panda nyasi zuia mmomonyoko wa udongo.

### KAULI YA MAZINGIRA YETU
IJUMAA, 30 JUNE 2023



"Ukosefu wa maji safi na salama unasababishwa na uharibifu wa mazingira uliokithiri. Hivyo kila mmoja wetu ashiriki kikamilifu kuhifadhi , kulinda na kutunza mazingira kwa ustawi wa vyanzo vya maji.

### KAULI YA MAZINGIRA YETU
JUMATANO, 28 JUNE 2023



"Vyanzo vya maji vinachafuliwa na maji taka kutoka viwandani na majumbani. Hii ni hatari kwa uhai wa binadamu na mazingira kwa ujumla. Hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kutoa taarifa pale atakapoona uchafuzi au uharibifu kwenye vyanzo vya maji.


### Kauli ya Mazingira yetu
ALHAMISI 13 JULAI, 2023



Namba 010

Ni wajibu wa kila mwekezaji kusajili miradi na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira ( TAM) ili kuepusha uharibifu wa mazingira na kumuwezesha kufikia malengo ya mradi. Zingatia kufanya TAM kwa manufaa ya mradi wako.

### Kauli ya Mazingira yetu
IJUMAA 14 JULAI, 2023



Namba 011

Uanzishaji wa miradi katika mipaka ya Kimataifa bila kufuata Kanuni za usajili wa miradi na makubaliano baina ya nchi zinazopakana huleta migogoro katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ni vema kusajili miradi ili kuepusha migogoro hii kwa ustawi na maendeleo ya Taifa.

## KAULI YA MAZINGIRA YETU


ALHAMISI 30, NOVEMBA 2023



Licha ya nyasi kuwa na faida lukuki katika kutunza mazingira lakini pia hutumika kama chakula cha mifugo kama vile ng'ombe. Panda nyasi kwa mustakabali wa maisha ya wanyama.

## KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMANNE 28, NOVEMBA 2023



Nyasi zinapooza hutengeneza mbolea na kurutubisha ardhi hali inayopelekea mimea kustawi vizuri shambani kutokana na mbolea hiyo. Hivyo panda nyasi rutubisha ardhi.

## KAULI YA MAZINGIRA YETU


IJUMAA 1, DESEMBA 2023



Aina ya nyasi kama ukoka hufanya mazingira kuwa na muonekano mzuri na wa kuvutia. Hivyo panda nyasi za ukoka pendezesha mazingira.

## KAULI YA MAZINGIRA YETU

ALHAMISI, 29 JUNE 2023



Uharibifu wa mazingira huathiri wingi na ubora wa maji, husababisha uhaba wa maji na na kupelekea mlipuko wa magonjwa kama kipindupindu. Hivyo tutunze vyanzo vya maji kwa ustawi wa afya zetu.

## KAULI YA MAZINGIRA YETU


JUMATATU, 26 JUNE 2023



Uharibifu wa mazingira huathiri wingi na ubora wa maji na kusababisha uhaba wa maji na kupelekea mlipuko wa magonjwa kama kipindupindu. Hivyo tutunze vyanzo vya maji kwa usawi wa afya zetu.

## KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMANNE, 27 JUNE 2023



Vyanzo vya maji ni rasilimali muhimu inayochangia maendeleo ya Nchi kwani tunapata maji kwa ajili ya kuzalisha nishati ya umeme, kilimo na shughuli za maendeleo. Hivyo tutunze na kulinda vyanzo vya maji.

## Kauli ya Mazingira yetu

JUMATATU 10 JULAI, 2023



Namba 007

Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) ni mchakato unaohusisha kutoa mapendekezo juu ya namna bora ya kupunguza athari kwenye mazingira zitokanazo na miradi. Hivyo sajili miradi NEMC kabla ya kuanza utekelezaji wake kuepuka athari kwenye mazingira.

## Kauli ya Mazingira yetu

JUMATANO 12 JULAI, 2023



Namba 009

Kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) humuwezesha mwekezaji kupata vibali mbalimbali vinavyohusiana na mradi wake, kukubaliwa kwa mradi wake na jamii (social license) na kuepusha migogoro baina ya jamii na mwekezaji. Hivyo ni muhimu kusajili mradi wako sasa.

*Wasiliana nasi;*
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**
Ghorofa ya 6, Jengo la Kambarage, Barabara ya PSPF S.L.P 2724, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 26 296 0098, +255 713 608 930
Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz

**#MazingiraYetuUhaiWetu**

Namba ya Bure: **0800110116**
@nemctanzania
NemcTVTanzania
www.nemc.or.tz